

## Maswali

1. Mungu aliyea Abramu jina gani mpya?
2. Jina Ibrahimu ina maana gani?
3. Mungu aliyea Sarai jina gani mpya?
4. Jina Sara ina maana gani?
5. Mungu alisema watoto wa Ibrahimu watakuwa namna gani?
6. Mbona Ibrahimu alikuwa na wasi wasi?
7. Nani walipita karibu na hema ya Ibrahimu?
8. Watu 3 walikuwa nani?
9. Walipea Ibrahimu ujumbe gani?
10. Ibrahimu na Sara waliita mwanaao eti nani?

## Majibu

1. Jina mpya lilikuwa Ibrahimu.
2. Ibrahimu ina maana Baba wa mataifa.
3. Jina mpya lilikuwa Sara.
4. Sara ina maana Binti wa Mfame.
5. Watakuwa wengi kama nyota za angani na mchanga ya pwani – hawawezi kuhesabiwa.
6. Ibrahimu hakukuwa na watoto tena Sara alikuwa mzee sana hangweza kuzaa watoto.
7. Watu 3 walipita.
8. Hawa watu walikuwa malaika wa kweli.
9. Walileta ujumbe kutoka kwa Mungu – Sara atapata mwana.
10. Waliita mwanaao eti Isaka.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

**Awamu ya 1 Mwaka wa 3**



## 5 Isaka anazaliwa

### Marejeo

Mwanzo 18:1 – 15 na 21:1 – 8

### Kiini cha somo

Kuonyeasha kwamba Ibrahimu aliamini Mungu hata kama ahadi ilionekana haitimizwi.

### Maneno maalum

- 5.1 Abramu 99 + majina yalibadilishwa + Ibrahimu + Sara + Mungu alifanya ahadi + watoto wengi +nyota
- 5.2 Ibrahimu ana wasi wasi + hakuna watoto + Sara mzee sana + Ibrahimu aliamini
- 5.3 Watu 3 + jipitishe + tulia na mpumzike + tengeneza chakula
- 5.4 Malaika + ujumbe kutoka kwa Mungu + Sara atapata mwana
- 5.5 Sara ana mwana + Isaka + furahi sana + shukuru Mungu

**5.1** Ibrahimu alipokuwa wa miaka 99, Mungu alimzungumzia tena juu ya ahadi alizokuwa amesema. Mungu alimwambia kwamba watoto wake na wajukuu wake watakuwa taifa kubwa. Mungu alimwahidi kwamba atamlinda yeye na watoto wake. Mungu aliahidi atawasaidia wakati watakuwa na huzuni au kwa shida. Mungu atatusaidia hata sisi pia kama tukimuuliza.

Mungu aliahidi Abramu na watoto wake nchi ya Kanaani (Israeli) pia. Mungu alibadilisha jina la Abramu likawa IBRAHIMU, kumaanisha BABA WA MATAIFA MENGI, kwa sababu Abramu atakuwa baba wa Wayahudi. Mungu alibadilisha jina la Sarai likawa SARA, kumaanisha BINTI WA MFALME – jina nzuri kwa mama wa taifa.



Mungu aliambia Ibrahimu kwamba watoto wake watakuwa kama nyota angani au changarawe ya pwani. Sidhani kama kunaye yeyote anaye weza kuhesabu hiso zote. Kwa hivyo Mungu aliahidi Ibrahimu wazao wengi.

**5.2** Ahadi hii ilimpa Ibrahimu wasi wasi sana kwa sababu Ibrahimu na Sara hawakuwa na mtoto yeyote! Sara alikuwa mama mzee na hangeweza kupata watoto kwa ajili ya umri. Ilikuwa miaka mingi imepita tangu Mungu afanye hiyo ahadi wakati alipokuwa akitoka Uru.

Ibrahimu aliamini mpaka Mungu atatimiza hiyo ahadi ingawaje hakuelewa ni jinzi gani. Alijua kwamba kila mara Mungu hutimiza ahadi zake, hata kama inaonekana haiwezigani kwa sisi.

**5.3** Siku moja, baadaye, Ibrahimu alikuwa anapumzika mbele ya hema yake chini ya kivuli cha miti ya mialoni. Alipokuwa amekaa chini ya miti, aliona watu watatu wanapita karibu naye.

Ibrahimu aliwambia wasiende ila wapumzike kwake na wale chakula pamoja naye. Bude tu, wote walianza kushugulikia chakula cha hao watu wakule.

**5.4** Lakini hawa watu hawakuwa watu – walikuwa malaika. Mungu alituma malaika 3 na ujumbe kwa Ibrahimu. Baada ya Ibrahimu kuwashugulikia na kuwapa chakula, walimpa ujumbe kutoka kwa Mungu. “Mwaka ujao Sara atakuwa na mwana.” Hapo Ibrahimu akajua kwamba wanatoka kwa Mungu na akasifu Mungu kwa sababu Mungu alikuwa ametimiza ahadi yake.



**5.5** Sara alipata mwana vile malaika walikuwa wamesema. Walimwita Isaka na wakawa na furaha sana kupata mtoto baada ya kungoja kwa muda mrefu. Walishukuru Mungu kumfanya Sara apate mtoto mvulana wakati ako mzee sana.